

## Learning by Ear

### "Everyone's Different – Respect for Minorities"

#### Episode 02: The Struggle for more Equality – Lois Auta from Nigeria wants to encourage other people with disabilities

**Author:** Katrin Gänsler

**Editors:** Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch

**Proofreading/Translation:** Tony Dunham

### Characters (O-Töne, Clips) / Narrators

<b><i>Narrator</i></b>		about 35	english
<b><i>Lois Auta</i></b>	female	31	english
<b><i>Mathilda Auta</i></b>	female	20	english
<b><i>Sergio Mainetti</i></b>	male	44	english
<b><i>Jamilah Hamza</i></b>	female	45	english

### Pronunciation:

Lois Auta (pronounced like German eu: leus)

Mathilda Auta (pronounced as written)

Sergio Mainetti (pronounced serdjio meinetti)

Jamila Hamza (pronounced like Djamila Hamza; like English zoo)

Gurgua (pronounced as written, G like German Gustav)

**Please note:** Walemavu hawaridhii kuitwa "**wasiojiweza**".

### **Intro:**

Karibu kwenye sehemu ya pili ya kipindi chetu cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kiitwacho, “**Kila mtu ni tofauti- Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**”. Katika kipindi hiki tutakutana na watu ambao hubaguliwa kwa sababu mbali mbali-kwa mfano watu wanaobaguliwa kwa sababu ya ulemavu wao. Leo, tuko nchini Naigeria ambako tunamtembelea Bibi Lois Auta mwenye umri wa miaka thelathini na mmoja. Bibi huyo anaishi kwenye chumba kidogo katika mji mkuu, Abuja. Kila siku anahitaji mtu wa kumsaidia kwa kuwa amekuwa akitumia kiti cha magurudumu tangu akiwa na umri wa miaka miwili. Hata hivyo, anasimamia maisha yake vilivyo na anataka sana kuwatie shime watu wengineo walemavu.

### **1. Sound: wheelchair-car**

### **2. Narrator:**

Dereva Isaak anakitoa kiti cha magurudmu kwenye gari lake kama ilivyo kawaida yake. Punde si punde ameshakiweka saawa ili Lois Auta apate kukikalia. Lois anamshukuru sana dereva wake kwa uvumilivu wake. Lau si yeye, Lois asingeweza kwenda kazini. Losi anatumia muda wa dakika 20 kufika kwenye jengo la Shirika la Kitaifa la Mafuta ya Petroli la Naigeria.

### **3. Sound: wheelchair**

#### **4. Narrator:**

Lois anakazana na kiti chake cha magurudumu. Jua linawaka kweli kweli; kwa hivyo huyu bibi analazimika kwenda akisimamisha kiti chake ili apumzike. Anasimamisha kiti chake kwa tahadhari kisha anajipangusa jasho. Hatimaye, anawasili ofisini kwake. Anafurahi mno japo ameumia vya kutosha kutokana na safari yake hiyo.

#### **5. Lois:**

*“Ninajitembeza mwenyewe kila mahali bila kutaka msaada wa mtu kwa kuwa ngazi zimo kila sehemu. Kuna ngazi zilizotengezewa walemavu. Kwa hivyo afisi yangu inawafaa sana walemavu. Wamezingatia maslahi yetu na wanatutunza vyema.”*

#### **6. Narrator:**

Jambo hili ni nadra kuonekana nchini Naigeria. Miongoni mwa raia zaidi ya milioni mia moja na hamsini wanaoishi Naigeria, watu kati ya milioni ishirini na milioni ishirini na mbili ni walemavu. Si sana kupata maslahi yao yakishughulikiwa ipasavyo. Jamilah Hamza anajua fika jinsi ambavyo maisha ya walemavu yalivyo magumu. Yeye hufanya kazi kwenye Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Naigeria. Hasa anashughulika na masuala ya walemavu katika shirika hilo.

## **7. Jamilah:**

*“Walemavu hawana uwezo wa kuingia kwenye majengo yetu mengi, majengo ya umma. Majengo mengi hayana ngazi maalumu za walemavu au kwezo. Kwa hivyo, ni vigumu sana kwa mlemavu mwenye magongo ya kutembelea au kiti cha magurudumu kwenda mathalani kwenye ghorofa ya tano. Hawezi kupata huduma zozote azitakazo zinazopatikana kwenye ghorofa hiyo.”*

## **KW begin**

## **8. Narrator:**

Nchi ya Naigeria iliidhinisha Mwafaka wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Walemavu mwezi Septemba mwaka elfu mbili na kumi. Mwafaka huo ulikusudiwa kuhakisha kwamba walemavu wangelindwa kisheria na kijamii kote duniani. Hata hivyo, nchini Naigeria mambo hayajabadilika vyovyote hata baada ya mwafaka huo kutiwa sahihi. Wanaohusika wanasubiri mswada wa sheria wa Naigeria ambao utashaghulikia malengo yaliyo kwenye mwafaka wa Umoja wa Mataifa. Hivi tunavyomtembelea Jamila Hamza ofisini mwake, mswada huo wa sheria ungali kwenye ofisi ya Rais Goodluck Johnson ingawa ulipitishwa bungeni mwaka 2001. Walemavu wataweza kutetea vyema haki zao za msingi pindi rais akiutia sahihi mswada huo kuwa sheria. Jamilah Hamza anasubiri hilo kwa hamu.

**9. Jamilah:**

*“Rais akishautia sahihi mswada huo walemavu watakuwa na haki zaidi za masomo, kutunzwa kiafya, haki ya kuingia kwenye majengo na pia haki ya kupata taarifa. Kwenye vituo vyote vya kitaifa vya televisheni-kama mjuavyo- kutakuwa na watu wanaotumia lugha ya ishara wakati habari zitakapokuwa zikipeperushwa hewani. Watu hao watakuwa wakiwafasiria habari jamii ya watu wasiosikia.”*

**KW end**

**10. Sound: keyboard**

**11. Narrator:**

Lois anakaa kwenye dawati lake na anachapa barua. Yeye ni mhazili wa Shirika la Kitaifa la Mafuta ya Petroli nchini Naigeria. Pia anasimamia magari ya shirika hilo. Kwa mfano, anahakikisha kwamba magari yanakarabatiwa mara kwa mara. Kazi hiyo anaifanya pamoja na wenzake wanne lakini leo yuko peke yake. Huku anapomalizia kuchapa barua yake, Lois anaeleza jinsi maradhi yalivyomkumba.

**12. Lois:**

*“Nilipotimia umri wa miaka miwili, nilipata homa na mama yangu akanipeleka hospitalini. Nilidungwa sindano hospitalini humo na baada ya hiyo sindano nikalala fofofu. Nilipoamka mama alinitaka niinuke nimeze dawa lakini sikuweza kusimama. Hapo ndipo ulemavu wangu ulipoanzia.”*

**13. Narrator:**

Alikuwa amekumbwa na maradhi ya kupooza ya Polio. Tangu wakati huo, Lois hawezi kutembea. Mama yake alilia machozi yakakauka. Baba naye aliwalaani madaktari kwa kuwa aliamini kwamba ndio waliosababisha ulemavu wa Lois. Hata hivyo alimpeleka binti yake shuleni. Losi alipomaliza masomo ya shule na akafanya mazoezi ya kazi ndipo alipopata kazi yake hii. Lois ana furaha si haba: mwaka huu anataka kuanza kusomea taaluma ya Usimamizi wa Umma. Anajua fika kwamba asingefikia kiwango alichofika bila msaada wa jamaa zake. Wazazi wake, ndugu zake wa kiume na dadake mdogo walimtia shie na pia kumlinda kutokana na ubaguzi. Lois anakumbuka kisa kimoja:

**14. Lois:**

*“Ninakumbuka siku moja mimi na ndugu yangu mdogo tulikuwa tumetoka shule. Mvulana fulani akaniita gurgua. Na gurgua katia lugha ya Kihausa ni msichana mlemavu. Ndugu yangu aliposikia hivyo alikasirika na akamwendea yule mvulana na akamuonya. Huyu mvulana hakuwahi kuniita hivyo tena.”*

**15. Narrator:**

Lois anachangamka sana anapokumbuka siku ambayo ndugu yake mdogo alipomtetea. Jambo hilo ni nadra kutukia. Mtoto mlemavu huonekana kuwa fedheha nchini Naigeria na pia kwenye mataifa mengine mengi. Jamilah Hamza anayefanya kazi katika Tume ya Kutetea Haki za Binadamu hukumbana na visa vingi sana vya ubaguzi:

**16. Jamilah:**

*“Kuna jamii nyingi zinazoamini kwamba walemavu husababisha mkosi. Wengine hufikia hatua ya kutaka kuwaua. Wasipowaua huwafungia majumbani mwao. Wanahisi: hii ni fedheha au laana, natumai unaelewa. Hawataki kuhusishwa nao. Nao walemavu wanapojitoa kimasomaso hudharauliwa sana: wanawekwa kwenye tabaka la chini.”*

**17. Narrator:**

Matokeo yake yanasikitisha. Walemavu hawana watetezi wao wala hakuna anayejali maslahi yao ila tu pale mtu anaposaidiwa na jamaa zake kama vile Lois anavyosaidiwa. Anataka kuondoka kazini mapema leo apelekwe chumbani mwake. Anaishi kwenye kambi ya kijeshi viungani mwa Abuja. Mjombake Lois alikuwa akikaa kwenye kambo hiyo lakini alihamishiwa kwenye eneo jengine. Lois aliruhusiwa kuishi humo bila malipo. Bahati yake kwa kuwa ni vigumu sana kupata nyumba za makazi mjini humo. Hata hivyo, bado anatatizika si haba kwenye kambi hiyo kutokana na ngazi nyingi zilizopo na ardhi ambayo si tambarare.

**18. Sound: wheelchair**

***KW begin***

**19. Narrator:**

Tatizo jingine ni kiti cha magurudumu cha Lois ambacho kimechakaa. Anahitaji jitihada za ziada kila anapokiendesha. Anatamani sana kigari cha umeme. Si rahisi kupata kigari hicho nchini Naigeria. Mkuu wa shirika la Christoffel-Blinden-Mission mjini Abuja, Sergio Mainetti, analeza:

**20. Sergio**

*“Hapa Naijeria tunapata tu viti vya magurudumu vilivyotengezewa Uchina. Katika kila duka unalokwenda, watakwambia: Naam. Tunaweza kukupatia kiti cha magurudumu: Vipi hali ya huyo atakaye kiti hicho? Ni mkubwa au mdogo, atakitumia hicho kiti wapi?”*

***KW end***

**21. Narrator:**

Lois anafika mlangoni pake. Si mwendo mrefu kutoka hapo kuingia ndani ya nyumba. Hawezi kusonga mbele kutoka hapa mlangoni. Anahitaji msaada.

**22. Lois:**

*“Siwezi kuingia ndani kwa sababu ya kipande cha zege kilichoko mlangoni. Hapana budi ila kukiinua kiti cha magurudmu ili nipate kuingia chumbani.”*

**23. Sound: call**

**24. Narrator:**

Kwa hivyo inambidi Lois kumpigia simu dada yake, Mathilda Auta. Anamsaidia Lois kwa kumuingiza nyumbani. Mathilda mwenye umri wa



miaka 20 ameshapika chajio. Anasoma somo la elimu-jamii lakini kwa sasa hivi yuko likizoni na anaishi na dada yake.

***KW begin***

**25. Mathilda:**

*“Ninamsaidia. Naam. Kwa mfano ninamfulia nguo. Kazi hizi za nyumbani. Ninapokuwa hapa kwake.”*

***KW end***

**26. Narrator:**

Lois anafurahia msaada huo. Hurudi akiwa amechoka sana baada ya kutwa nzima ya kazi. Kutokana na uchovu alio nao, Lois anajiagusha kwenye godoro sakafuni. Mathilda anamletea chupa ya maji. Anasema huku akielekea jikoni:

**27. Mathilda:**

*“Kusema kweli, yeye ni mtu mwenye bidii. Anataka kila jambo analolifanya alifanye vizuri zaidi.”*

**28. Narrator:**

Hata hivyo, kuna jambo ambalo Lois hajaliafikia ingawa anatamani sana: anataka kupata watoto na anatamani kumpata mwanamume atakayempenda kwa dhati. Anatamani kuwa na familia yake. Miaka kadha iliyopita alidhani kwamba ametimiza ndoto yake lakini mambo yakavurugika. Anakumbuka:

**29. Lois:**

*“Nilichumbiana na mwanamume fulani kwa muda wa miaka mitatu. Mwanamume huyo alinipenda sana na akanipeleka kwao kunitambulisha kwa jamaa zake. Mara tu tulipowasili kwao, wazazi wake wakanifurusha. Walimuuliza alikuwa amekosa nini hata aamue kuo a mlemavu? Sidhani kama tutaweza kuoana wazazi wake wakiwa bado hai.”*

**30. Narrator:**

Hata hivyo Lois Auta hajakata tamaa kupata mwanamume wa kumuoa. Anachukia sana ubaguzi. Lois anataka kuwathibitishia wanaume kwamba na yeye ni binadamu sawa na binadamu wengine.

**31. Lois:**

*“Wanaume wengi huchukulia kuwa wanawake kama sisi hatuwezi kutunza nyumba vyema. Wengine hufikiria kwamba hatuwezi tend la ndoa. Tunaweza kama binadamu wengine. Tena huenda tuna ujuzi kuwashinda wengine. Kwangu mimi, sisi ni mabingwa wa kutunza nyumba.”*

**32. Narrator:**

Lois ana lengo jingine zaidi ya kuwa na familia yake: angetaka raia wanachi yake wamthamini zaidi wala wasimchukulie tu kuwa mwanamke mlemavu wa kusikitikiwa kila uchao. Daima anathibitisha kuwa anajikimu kimaisha.

**Outro:**

Leo tumekutana na Lois Auta anayetoka Abuja. Tunatumai umefurahia mazungumzo ya msichana huyo ambaye anaendesha maisha yake vyema ingawa ni mlemavu. Aliyetuletea taarifa hii ni Katrin Gänslar.

Ikiwa unataka kujua jinsi watu wa jamii za walio wachache wanavyotendewa barani Afrika, sikiliza kisa hiki na visa vinginevyo vya kipindi chetu cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**. Unaweza pia kufungua tovuti yetu [www.dw.de/lbe](http://www.dw.de/lbe). Tunakushukuru kwa kututegea. Usisahau kususikiliza tena kwenye sehemu ijayo. Kwaheri.